# LEARNING BY EAR

## ”WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA”

## EPISODE ONE: ”IT’S A BABY BOY!!!”

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: Katrin Ogunsade**

**Health Expert: Dr. Heidrun Hübner**

**List of characters for episode 1:**

- MASIKA (40),
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- MAMA DAVID (43)
- ZAWADI (INFANT, actor not needed)
- DR. MUNGA (45)
- RADIO PRESENTER (28)
- NARRATOR/Intro/Outro (same person)

**INTRO/NARRATOR:**

Hujambo msikilizaji na karibu tena katika kipindi cha Learning By Ear Noa Bongo jenga maisha yako.Ni mchezo wa radio kuhusu ugonjwa wa Malaria kwa jina ''**Wageni vizabizabina –Msoalikwa. Katika mchezo huu tutasikia jinsi Familia moja inavyoanzisha vita dhidi ya Malaria. Bila shaka msikilizaji** umepoteza wapendwa wengi kutokana na malaria. Katika mchezo huu ,Yote yalitokea mwaka huu ambapo ulikuwa ndio mwaka wa Karembo kumaliza elimu yake ya masomo ya msing**i.Tega sikio.**

**SCENE ONE: EVENING (8.00PM) AT MASIKA'S HOME**

**(KAREMBO IS DOING HER HOMEWORK IN THE LIGHT FROM A KEROSENE LAMP)**

**A-SFX: SOUND OF CRICKETS, MOSQUITOS, OTHER NIGHT ANIMALS, burning sound of kerosene lamp**

1. **KAREMBO:** (Speaking to the lamp)tafadhali.. tafadhali nakurai usizimike... jikakamue mpaka nitakapomaliza kazi zangu za shule...
2. **B-SFX: (SHAKES LAMP TO CONFIRM ITS EMTPY – MATCH STICK BEING LIT…)**
3. **KAREMBO:** Mungu wangu! Taa imezima? Nitamalizaje kazi zangu za shule? ( **CALLS OUT**) baba!!!! baba!!
4. **MASIKA**: (**RESPONDS SLEEPILY**)kunani?

5. **KAREMBO**: samahani kwa kukuamsha,lakini taa imezima na bado sijamaliza kazi zangu zashule..

6. **MASIKA**: Basi kalale.. kwanza kumekuwa usiku mwingi...

7. **KAREMBO**: Wenzangu watanipita... nahitaji kumaliza kazi za shule kwanza ndio nilale..

8. **MASIKA**: Hujawahi kupata nambari chini ya tano tangu ulipoanza chekechea... nina hakika utafuzu pia mwakani...

9. **KAREMBO**: Nafahamu... lakini nisipojizatiti sitafaulu... tafadhali nipe

pesa nikimbie dukani kununua mafuta kabla vibanda havijafungwa...

10. **MASIKA**: (**GETTING AGITATED**)

sina pesa! Ala!! Mimi ni mvuvi,na sio mkurugenzi wa Benki! Unafahamu vyema kuwa senti chache nilizopata baada ya kuuza samaki tumezitengea mamako kwani muda wowote atatuletea mgeni... zinahitajika hospitali na hapa pia.. ( AKIGEUZA SAUTI)kwanza yeye mwenyewe yuwapi? Amekwendapi? Usiku umeshaingia yeye ni kiguu na njia tu kama aliyekula miguu ya kuku!

11. **KAREMBO**: Sijui... labda bado yuko kwa mamake david...

12. **MASIKA**: Wanawake bwana! Mchana kutwa hauwatoshi kusengenyea? Nenda ukamwite! Mara moja! Na ukifika huko muulize mama david atukopeshe mafuta taa....

13. **KAREMBO:** Ndio baba...

14. **NARRARTOR**: katika kiza tororo alinyatuka msichana huyo Karembo... mastakimu ya mama david yalikuwa pua na mdomo na pale pao.. baada ya dakika za kutema mate yasikauke aliweza kuona kibatari chao kikiwaka kwa mbali..

**<u>SCENE TWO: AT MAMA DAVID'S HOUSE</u>**.

15. **C-SFX: KNOCKS AT THE DOOR.**

16. **MAMA DAVID:** Nani huyo?

17. **KAREMBO:** Ni mimi karembo

| | | |
|---|---|---|
| **18.** | **MAMA DAVID:** | Oh Karembo,Ingia... nilidhani ushalala saa hizi... mwanangu david alilala kitambo saa nzima yapata.. |
| **19.** | **KAREMBO:** | Labda alimaliza kazi zake za shule mapema.. mimi sikuweza kwa ajili taa ilizima kabla nimalize.. |
| **20.** | **MAMA DAVID:** | **(SURPRISED)**<br>Kazi za shule? Kazi gani? David hajasubutu kunieleza chochote kuhusu kazi hizo... mtoto huyu ni mvivu mno! Ndio daima anapata alama duni shuleni! Siku zote kuzembea kwake kumetushusha amasa mimi na marehemu babake.ametutia aibu! |
| **21.** | **KAREMBO:** | Mama... baba amesema eti... |
| **22.** | **BETTINA:** | Najua hataki kuniona nimetoka hapo nyumbani.. kwaheri mamake david na asante kwa ushauri... haya turudi karembo ongoza njia...( AKIHEMEA JUU JUU ) ah.. huyu mtoto ashanichokesha... |
| **23.** | **KAREMBO:** | Hmm ( AKIONA AIBU ) mama.. pia baba alisema vile mafuta ya taa yamekwisha... tu.. tu... |

**24. MAMA DAVID:** Karembo,Mwanangu... usione haya kwa hayo...kusaidiana ni kawaida kwa majirani kama sisi...subiri nikuletee mafuta taa....

**25. BETTINA:** (**HUSHED WHISPER)**
kwani babako hana pesa hata za kununua mafuta ya taa?

**26. KAREMBO:** (**ALSO WHISPERS)**
hana.. anasema pesa zote alizochuma amekuwekea wewe wakati...

**27. MAMA DAVID:** **(CUTS IN THEIR CONVERSATION)**
haya chukuwa... yatakuokoa kwa muda wa siku chache...

**28. KAREMBO:** Asante mama david..

**29. BETTINA:** Nashukuru... asante sana.. na upate usingizi mwanana.

**30. MAMA DAVID:** Nanyi pia mlale vyema.. usishau tuliyozungumza...

**31. D-SFX: DOOR OPENS THEN SHUTS...LATER BOLTED**

**(KAREMBO AND HER MUM HEADING HOME)**

**32. BETTINA:** Ala! Karembo.. Hebu twende taratibu usifulize kama unayechapwa kwa ufito na mwenzio wanaiona haliniliyo... (**TAKING SHORT BREATHES)**

**33. KAREMBO**: Samahani mama.. naharakisha kumaliza kazi za shule.. lakini mama utajifungua lini?

**34. BETTINA:** Yani hujui? Hata haya huoni? Na kesho utakuwa mama kama mimi? Ni lazima ujijuwe na ujuwe mambo ya mwanamke yote!huu ni mwezi wangu wa tisa.. mwezi wangu wa mwisho... kwa hivyo muda wowote nitapata uchungu wa kuzaa...

**35. KAREMBO:** Je unadhani atakuwa mtoto wa kiume au wa kike?

**36. BETTINA:** Siwezi kujua.. watoto ni baraka kutoka kwa Mungu.. kwahivyo mtoto ni mtoto awe wa kike au wa kiume... wote ni sawa.

**37. KAREMBO:** Afadhali tumefika nyumbani...mama subiri nifunguwe mlango...

**38. E-SFX: DOOR OPENS…THEN SHUT**

**39. BETTINA:** Heee!Na hapa ndani panatisha kwa hiki kiza...

**40. F-SFX: SOUNDS OF BUZZING MOSQUITOES.**

**41. KAREMBO:** Na hawa wageni wetu wasoalikwa.. wanaonekana na njaa sana...na vile nachukia hizo sauti zao...

**42. BETTINA:** (**DEEP PAINFUL CHILD-BEARING CRY)**
Oooooooh!.... aaaaaaaaaah!

**43. KAREMBO:** (**SHOCKED)**
mama.. una nini? Unaumwa?

**44. BETTINA:** **(IN APPARENT LABOUR PAINS)**
hebu niitie babako... muite! Mwambie nahisi uchungu umewadia!!!! (**ANOTHER CRY)**

**45. KAREMBO:** **(IN A SHOCKED VOICE)**
baba! Amka! Amka baba!!!

**46. MASIKA:** **(NOT HAPPY)**
Haya kuna nini tena?

(**YAWNS AND STRETCHES)**

**47. BETTINA:** Aaaaaaaaaah… Haraka!!!!!
**(BETTINA LETS OUT ANOTHER PAINFUL CRY)**

**48. KAREMBO:** Ni mama.. amesema anahisi uchungu... anataka kujifungua...

**49. MASIKA:** Sasa? Mbona hamukuniambia mapema? Subiri... mama karembo.. naja! (AKISEMA HARAKA) Humu namo muna giza mno! Unaweza kutembea?

**50. BETTINA:** **(PAINFULLY SPOKEN IN BETWEEN BREATHS)**

La! Sidhani.. siwezi...

**51. MASIKA:** Karembo.... Hebu mtupie jicho mamako naenda kutafuta usafiri tumpeleke hospitali... kukitokea chochote muite mama david aje kumsaidia mamako...

**NARRATOR:**kwa kudura za Mungu hakuna patashika yeyote iliyojiri.. mambo yalikwenda mchakamchaka na kwa kasi ya chui mwindaji masika alirudi nyumbani kwake na kumpeleka mkewe betina hospitali... Karembo alisahau kamwe kuhusu kazi zake za shule na badala yake aliichukua redio ya babake na...

**<u>SCENE THREE: RADIO PROGRAMME</u>**

**52. G-SFX: RADIO BEING TUNED**

| | | |
|---|---|---|
| **53.** | **PRESENTER:** | karibu msikilizaji katika kipindi chetu cha kila wiki... ” maisha bora” leo katika kipindi chetu tunae Daktari Munga wa hospitali ya wilaya ya Ribo atakayetuzungumzia hoja hii ya malaria na athari zake katika jamii yetu. Karibu |
| **54.** | **DR. MUNGA:** | Asante na hamjambo wasikilizaji... |
| **55.** | **PRESENTER:** | Daktari.. hebu tutandikie jamvi letu leo hii kwa kutufahamisha maelezo kuhusu malaria.. Ni nani hasa adui huyu anayeitwa malaria? |
| **56.** | **DR. MUNGA:** | **(CLEARS THROAT)**<br>ah.. malaria ni ugonjwa hatari unaosababishwa na vidudu haswa mbu wakike anayeitwa anoflesi.. Mtu yeyeto anayeumwa na mbu huyu anaweza kuambukizwa kwa kuwa anategemea damu ili kupata uhai na kutaga mayai yake.. |
| **57.** | **PRESENTER:** | Unasema malaria inahatarisha maisha? |
| **58.** | **DR. MUNGA:** | Ndio, kama haitatibiwa kwa wakati ufaao na dawa zinazofaa, inaweza kuua mtu baada ya siku chache anapopata ugonjwa huu..kwa hiyo kuwa mwangalifu sana unapoonyesha |

ishara za homa na kisunzi kwa muda wa zaidi ya siku mbili.Hadi sasa hakuna chanjo dhidi ya malaria.

**59. PRESENTER:** Na ulisema kuwa mtu yeyote anaweza kuambukizwa lakini niweke wazi na pia wasikilizaji waweze kuelewa.. ni nani au ni watu gani haswa walio katika hatari zaidi ya kuambukizwa na kwanini?

**60. DR. MUNGA:** (**CLEARS THROAT AGAIN)**
Kusema kweli.. takwimu zinaonyesha kuwa asilimia arobaini ya jumla ya watu duniani wako katika hatari hiyo ya maambukizi... lakini wale walio katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa malaria ni akina mama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano... hii ni kwa sababu kinga yao ya mwili huwa iko chini.... hivyo kuathirika...

**61. KAREMBO:** Asilimia arobaini? (**SHOCKED)**
hiyo ni takriban nusu ya ulimwengu mzima sasa!

**62. DR. MUNGA:** (**CONTINUES)**
si hayo pekee.. ripoti zinaeleza kuwa katika kila sekunde thelathini kuna mtoto anayefariki kutokana na malaria au maradhi mengine yanayotokana nayo....**(BAD RECEPTION)**

**63. (SILENCE AS BATTERIES DIE)**

**64. KAREMBO:** (**DISAPPOINTED)**
Ah! Haya mawe yamekufa nguvu wakati somo limepamba moto!..kwahivyo ni mbu anoflesi anayesababisha malaria,alafu.. asilimia arobaini ya watu duniani wako katika athari ya maambukizi, na kila sekunde thelathini... ati kila sekunde thelathini mtoto anafariki? Hayo ni maafa makubwa!. (**REALISES IT'S LATE)** imetimu karibu sa sita usiku.. nahitaji kulala...

**65. H-SFX: BLOWING OUT LAMP. MORE BUZZING SOUNDS OF MOSQUITOES. FOLLOWED BY A NUMBER OF SLAPS TO KILL THEM.**

**KAREMBO:**Niwacheni nilale nyinyi mbu anoflesi! Niwacheni !

(**MUSIC BRIDGE)**

**MASIKA:** (**EXCITED AND HAPPY)**

Karembo!!,Karembo!!Ni mtoto wa kiume .. tumemwita Zawadi!!!

**NARRATOR:** Kwa takriban miaka kumi na nne aliyonayo Karembo hajawahi kumuona babake akiwa mcheshi kama alivyo sasa! Hata katikati ya kiza bado aliweza kuiona tabasamu iliyotanda kinywani kwa babake,furaha ilibubujika. Lakini hakujuwa au tuseme hawakujuwa kuna mengi yanayokuja baada ya mwanzo huo wa furaha...Usikose kujiunga nasi wiki ijayo katika sehemu ya pili ili utambue ni kipi kitakachotokea katika mchezo huo kwa jina wageni vizabizabina Msoalikwa.Kumbuka pia unaweza kutuandikia maoni yako au kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia tovuti www.dw-world.de/lbe

Hadi wakati mwengine..Kwaheri.